MINISTRY OF AGRICULTURE TRAINING ANDEXTENSION SERVIC
ROMAN CATHOLIC CHURCH DIOCESE OF NJOMBE
MAMRE AGRICULTURE AND LIVESTOCK COLLEGE
P.O. BOX 50, ILEMBULA,
Contact: +255 750793604
Email: mamrecollege01@gmail.com
Websites: www.mamre.ac.tz



**JINA KAMILI: ……………………………………………………**
**NAMBA YA SIMU:…………………………………………………………..**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KWA MWANAFUNZI NA CHUO CHA KILIMO NA MIFUGO MAMRE 2026/2027**

Ndugu napenda kukutaarifu na kukupongeza kwa kuweza kuchaguliwa kujiunga na chuo cha Kilimo na Mifugo Mamre kwa mwaka wa masomo 2026/2027. Umechaguliwa kusomea kozi ya kilimo na mifugo katika ngazi ya cheti (Certificate in Agriculture Production).
Tafadhari soma maelekezo kwa umakini

**1.0 Tarehe ya kufika na kuripoti**
Chuo kitafunguliwa tarehe 15/10/2026, Hivyo unaombwa kuripoti siku hiyo na utapokelewa na utawala wa chuo na kusajiliwa. Ukishindwa kuripoti ndani ya wiki tatu (3) baada yakufungua hutapokelewa na utahesabika umeshindwa kujiunga na chuo.

**2.0 Usafiri**
Utahusika na gharama zote za usafiri kutoka nyumbani mpaka chuoni na kurudi wakati wa likizo.

**3.0 Mahali chuo kilipo**
Chuo cha Mamre kipo karibu na njia panda ya kwenda Ilembula hospitali/Halali wilaya ya Wanging'ombe, mkoa wa Njombe njia kuu ya kwenda Mbeya ukitoka mji wa Makambako. Umbali kutoka barabarani ni 0.5Km.
i. **Kwa Ngazi ya Cheti (Certificate in agriculture production)**
Mwanafunzi atalipa ada ya Tsh. **1,000,000** kwa mwaka na italipwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo: Awamu ya kwanza Laki sita **(600,000)** na Awamu ya pili
Laki nne (**400,000);** Ada yote inapaswa iweimelipwa mwanzo wa kila Muhula.



CS CamScanner

ii. **Kwa ngazi ya stashahada (Diploma in Agriculture Production**)
Mwanafunzi atalipa ada ya Tsh. **1,200,000** kwa mwaka na italipwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo: Awamu ya kwanza Laki (600,000) na Awamu ya pili Laki sita (**600,000);** Ada yote inapaswa iwe imelipwa mwanzo wa kila Muhula.
Malipo yote ya Ada yafanyike katika benki ya CRDB kwenye akaunti namba ***0150472870900*** jina la akaunti ni MAMRE AGRICULTURE AND LIVESTOCK COLLEGE na risiti ya malipo iwasilishwe chuoni.

**5.0 Malazi**
Chuo kinatoa huduma ya malazi katika mabweni yake yaliyopo hapa chuoni. Mabweni yote yana vitanda na magordoro. Chumba kimoja kinaweza kubeba wanafunzi wanne kwa wakati mmoja. Hairuhusiwi kitanda kimoja kutumiwa na wanafunzi wawili na hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kukaa nje ya mabweni ya Chuo. Wanafunzi wanashauriwa kuja na nguo nzito kwaajili ya kipindi cha baridi kinapofika.

**6.0 Mahitaji**
Mwanafunzi atapaswa kuja na vitu vifuatavyo siku atakayokuwa anaripoti chuoni
**Kwa ajili ya mwanafunzi mwenyewe**

i. Mashuka 2
ii. Blanketi 1
iii. Mto wa kulalia
iv. Chandarua
v. Mavazi ya michezo (Track suit)

**Kwa ajili ya mafunzo**
i. Ndoo 2
ii. Jembe la mkono na mpini wake
iii. Fagio laini 1 na chelewa 1
iv. Panga 1
v. Rim paper 2
vi. Daftari
vii. Peni, Penseli, Rula na mfutio
viii. Mkebe
ix. Scientific calculator 1
x. Passport 2 za rangi kwaajili ya kitambulisho na vyeti(20,000)
xi. Hela ya kitambulisho 10,000
xii. Maktaba 10,000 kwa mwaka

xiii. Serikali ya wanafunzi 15,000
xiv. Hela ya NACTE 20,000
xv. Hela ya Bima ya afya 55,000 (ni lazima kama huna bima)
xvi. Koti la maabara moja (jeupe) na koti la kazi za nje (dark blue)
xvii. Gumboots pair (1)
xviii. Hela ya tahadhari 20,000 (hairudishwi)
xix. Hela ya kujikimu (pocket money)
xx. Hela ya t-shirt ya Chuo 20,000ROMAN CATHOLIC CHURCH DIOCESE OF NJOMBE
xxi. HOSTEL 100,000

**7.0 Nidhamu**

Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na tabia nzuri na kujiheshimu akifuata na kuheshimu sheria na taratibu za Chuo. Muda wote awe nadhifu na avae nguo za heshima. Haturuhusu vimini, suruali za kubana, suruali zilizo chanwachanwa wala uvaaji wa Kata K. darasani hairuhusiwi viatu vya wazi, Mwanafunzi atakabidhiwa nakala ya
sheria na taratibu za Chuo pale atakapowasili.

**8.0 Usajili**

Wakati wa usajili kila mwanafunzi atapaswa kuleta cheti orijino cha fomu 4 na Matokeo ya mtihani kwa wanaoingia diploma. Kila mwanafunzi atapasika kuja za fomu maalumu ya taarifa zake wakati wa usajili

**9.0 Umakini katika masomo**

Ili mwanafunzi aweze kuhitimu ana hitajika kufaulu mitihani yote anayofanya. Wanafunzi wanashauriwa kusoma kwa bidii na kujua mwongozo wa majaribio ya mitihani.

**10.0 Mafanikio ya chuo**

Chuo kimetoa wanafunzi wengi walioendelea na masomo ya chuo kikuu baada ya kuhitimu ngazi ya diploma na wengine kuajiriwa na serikali pamoja na taasisi mbalimbali.

**11.0 Gharama za chakula**

Chakula kinapatikana kwenye cafeteria (mgahawa) wa chuo kwa gharama za mwanafunzi mwenyewe.

……………………………..

IRENIO L. MTITU
MKUU WA CHUO
KARIBU CHUO CHA KILIMO NA MIFUGO MAMRE.
(KILIMO NI BIASHARA)



CamScanner